

**Minutes of meeting of Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
25 April 2009**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Amos Sindano  
Bashiri Rashidi  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Juma Ali Salehe Jongo  
Mohammed Samwely

**Mradi wa Wamba**

Elaine alimtumia email kwa Una Osili kumjulisha kwamba tumepata hela.

Kwenye mpango wetu tuna mpango kufundisha wapanda baisikeli 60 wa kawaida (siyo wanafunzi wa shule). Tuliambia kujaribu kupata shule ambapo tunaweza kutumia darasa na viwanja siku za jumamosi – wanachama walipendekeza shule ya Mwembe Chai, Magomeni au shule ya Mpakani, Mabibo. Tutatengeneza vipeperushi kupata wapanda baisikeli kujiandikisha kufanya mafunzo jumamosi mbili. Elaine atatayarisha barua kwa shule kuomba kutumia darasa na uwanja.

Amos atatengeneza video ya mafunzo.

Pia tuna mpango kufundisha waalimu wa udereva. Elaine alimpigia simu Bwana Wamba wa chuo cha usafirishaji. Yupo Arusha na alipendekeza tukutane naye tarehe 5 mei baada ya kurudi.

**Kongamano / JICA**

Juma ataendelea kufuatalia.

**Re-cycle**

Elaine atatayarisha barua kwenda TRA kuomba namba ya TIN na Juma ataipeleka. Elaine atatayarisha barua kwenda kwa Mkuu wa Wilaya wa Kinondoni kuomba barua kwa TRA kupata msamaha wa kodi na Juma ataipeleka. Elaine atatumia email kwa Re-cycle kuomba barua kutoka kwao na cheti chao cha usajili.

**WHO mkutamo wa usalama wa barabara**

Mejah sasa ana visa na tiketi. WHO aliomba afanye maada kuhusu kuhamasisha serikali kuhusu usalama wa barabara kwa wapanda baisikeli. Elaine na Mejah wataandaa maada na wataleta kwenye mkutano ili wanachama wapitie.

**Wimbo**

Elia hakuweza kuhudhuria mkutano lakini alipiga simu wakati wa mkutano akasema anaendelea kutengeneza single.

### **Fasta Cycle couriers**

Mejah aliongea na Bwana Bukuku na ana appointment kumwona wiki hii kupata taarifa kuhusu vipi tutaendelea kuanzisha ushirika.

### **Siky ya Muungano**

Juma alienda kufanya mazoezi pamoja na CHABADA kutayarisha kwa msafara wa siku ya muungano, na atashiriki pamoja na wapanda baisikeli wa CHABADA kesho. Tuliuliza kama wanachama wengine wataweza kushirika lakini CHABADA walisema lazima washiriki ni wao waliohudhuria mazoezi basi haitawezekana.

### **Vodacom**

Juma alipeleka barua kwa Vodacom kuwapongeza kuhusu kampeni ya matangazo ya usalama barabarani inayotamka wapanda baisikeli.

### **Ruzuku ya Foundation for Civil Society**

Elaine alipata CVs za waalimu wa kompyuta. Atakuja na documents zote wiki ijayo ili tupitie na tutumie kwa FCS.

### **Video ya usalama wa baisikeli**

Elaine alileta CDs 20 pamoja na stika. Alinunua CDs 30 kwa Tsh 500 kila moja bila kesi.

Paulo alisema kwa simu kwamba alipima DVD na ilifanya kazi vizuri.

Amos alipata taarifa kuhusu gharama za CDs, DVDs, stika na kesi. DVDs ni Tsh 1,000 bila kesi. Kesi ni Tsh 500. Stika ni Tsh 400 (hana uhakika kama ni ya kurasa ya stika mbili au ya stika moja). Sanduka la stika ni Tsh 26,000 (hana uhakika kuna stika ngapi ndani).

Tulikubali Juma anunue kesi 28 za CDs wiki hii ili CDs tunazotoa ziwe na kesi.

Elaine atatayarisha barua kwa stesheni za TV (TBC1/TVT, ITV, East Africa TV, Channel 10) na kwa shirika tunawasiliana nao kwenda pamoja na CD au DVD.

### **Kiingereza**

Juma, Filbert, Kibwana, Ally Athman na Shamte walihudhuria mafunzo ya kiingereza wiki jana. Mwalimu hajupo wiki hii.

### **Hela na guta**

Ramadhan alitumia Tsh 14,000 ya hela ya guta kwa kupitia Bashiri na bado anadaiwa Tsh 7,000. Elaine alirudishiwa Tsh 15,000 aliyotumia kwa CDs. Juma sasa ana Tsh 14,000 ya hela ya UWABA.

**Mambo mengine**

Rafiki wa Filbert anaitwa Issa anayepanda guta alipata ajali. Filbert anajaribu kupata taarifa zaidi kuhusu hali yake na yupo wapi.